THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE

NATIONAL FRAMEWORK COORDINATION MECHANISM FOR TACKLING ILLEGAL MARITIME ACTIVITIES 2022

UHURU
NA
UMOJA

Yaliyomo

Yaliyomo ii
Tafsiri ya misamiati..... iii
Dibaji iv
1. TANGULIZI 1
1.1 Eneo la Bahari 1
1.2 Matarajio ya mwongozo 2
2. MAONO, UPEO NA LENGO LA MWONGOZO 2
2.1 Maono 2
2.2 Upeo 2
2.3 Malengo na maeneo ya kipaumbele..... 3
3. SHUGHULI HARAMU KATIKA UKANDA WA BAHARI NA MAJI YA NDANI 3
3.1 Shughuli haramu zinazofanyika 3
3.2 Kupunguza shughuli haramu bahari na maji ya ndani 4
4. URATIBU 4
4.1 Sera na Sheria 4
4.2 Kubadilishana habari na uzoefu 4
4.3 Shughuli za pamoja..... 5
4.4 Mazoezi ya pamoja 5
4.5 Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Baharini 5
5. USIMAMIZI WA MWONGOZO..... 5
5.1 Msimamizi mkuu 5
5.2 Majukumu na Wajibu wa Kamati yaTaifa ya Usalama wa Baharini 6
5.3 Wajibu na majukumu ya vyombo vingine 6
5.3.1 Shirika la Wakala wa Meli Tanzania na Kituo cha Kupashana Habari 7
5.3.2 Mashirika ya Utekelezaji wa Sheria ya Bahari 7
5.3.3 Mashirika mengine yanayoshiriki 8
6. UFUATILIAJI, TATHMINI NA MAPITIO YA MWONGOZO..... 10
6.1 Ufuatiliaji na Tathmini..... 10
6.2 Mapitio ya Mwongozo 10
6.3 Maandalizi ya Kanuni na Taratibu za Uendeshaji..... 11
Kiambatisho cha 1: Orodha ya vyenzo zinazohusika kwa utekelezaji wa mwongozo.... 12
Kiambatisho cha 2: Orodha ya Wizara, Idara, na Taasisi Zinazohusika katika Utekelezaji wa Sheria za Baharini..... 14
Kiambatisho cha 3: Orodha ya Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika Mengine yanayoshiriki katika utekelezaji..... 14
Kiambatisho cha 4: Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mwongozo 15

Tafsiri ya misamiati

Ukanda wa Pekee wa Kiuchumi – maana yake ni ukanda wa baharini uliofafanuliwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Bahari ya mwaka1989.

Shughuli Haramu za Baharini – maana yake ni matukio yanayotokea au shughuli zinazofanywa katika eneo la bahari au kandokando mwa bahari zinazotishia usalama wa maisha, mazingira ya baharini na ustawi wa kijamii na uchumi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maji ya Ndani – ina maana sawa na ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 303 cha Sheria ya Usafirishaji wa Meli za Kibiashara, 2003; Aidha, inajumuisha maji ya ndani yaliyopo katika maziwa na mito iliyopo upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maji ya Pwani – maana yake ni maeneo yote ya bahari ambayo yako upande wa nchi kavu mwa Bahari ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kupunguza – maana yake ni hatua ya kupunguza madhara ya shughuli haramu baharini.

Shughuli haramu za bahari – maana yake ni shughuli zinazofanyika baharini kinyume cha Sheria.

Miliki ya Bahari – maana yake ni ukanda wa baharini uliofafanuliwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Bahari ya mwaka 1989 inayohusu eneo halali la bahari linalomilikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dibaji

Tanzania ni nchi ambayo iko katika mwambao wenye rasilimali nyingi za baharini katika ukanda wa pwani ambazo zinahitaji ulinzi dhidi ya shughuli haramu za baharini kwa maslahi ya taifa. Ili kuimarisha usalama wa baharini ulinzi wa rasilimali za baharini Serikali imefanya juhudi kadhaa ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini, Timu za Wakala mbalimbali na pia kutia saini na kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa. Kwa miaka mingi shughuli haramu za baharini zimeendelea kuripotiwa katika eneo la bahari na maji ya ndani ikiwa ni pamoja na uharamia, biashara ya madawa ya kulevya, biashara ya binadamu, utoroshaji wa maliasili na uvuvi haramu.

Kuendelea kufanyika kwa shughuli hizo ni kwa sababu ya kukosekana kwa mwongozo madhubuti wa kuzuia na kukabiliana na shughuli haramu za baharini ambao unaainisha wajibu na majukumu ya vyombo vinavyohusika na udhibiti, ulinzi na usalama katika eneo la bahari na maji ya ndani. Kutokana na kukosekana kwa mfumo au utaratibu wa kujitosheleza wa uratibu, shughuli nyingi haramu za baharini katika eneo la bahari hazijashughulikiwa ipasavyo hivyo kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha upotevu wa rasilimali za bahari na kudhoofisha juhudi za kitaifa za kupunguza umaskini.

Kutokana na kuendelea kutokea kwa shughuli haramu za baharini katika eneo la bahari la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Uhalifu wa Dawa za Kulevya (UNODC) imeandaa Mwongozo huu wa Kitaifa wa Kukabiliana na Shughuli Haramu za Baharini ili kuimarisha uratibu, udhibiti na usalama katika eneo la bahari na maji ya ndani ya nchi (maziwa na mito).

Mwongozo huu umeandaliwa kushughulikia mahitaji ya sasa na kubainisha taasisi zinazohusika na uratibu, udhibiti na usalama katika eneo la bahari na maji ya ndani na unaainisha majukumu ya kilataasisi, utaratibu wa kubadilishana habari na kutoa tathmini ya utendaji na mapitio ya mwongozo huu.

Dkt. John A. K. Jingu
KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
(SERA, BUNGE NA URATIBU)

1. TANGULIZI

1.1 Eneo la Bahari

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya Afrika Mashariki inayopatikana kando ya ukingo wa magharibi mwa Bahari ya Hindi na Eneo lake Pekee la Kiuchumi lina urefu wa zaidi ya kilomita za mraba 240,000, kati ya latitudo 4º 40' 42"K na 7º 12' 39.1" K na longitudo 38º 32' 15.5"M na 43º 16' 56.1"M. Pia, Tanzania ina jumla ya eneo la maji ya ndani ambalo lina ukubwa wa kilomita za mraba 62,000 linalojumuisha vyanzo vinne vya maji vya Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na Rukwa. Rasilimali hizi hutoa fursa za uwekezaji katika uvuvi mdogo mdogo na uvuvi wa bahari kuu, nishati mbadala, bioteknolojia ya baharini, uchimbaji wa bahari kuu, uvunaji wa chumvi, utafutaji wa rasilimali za mafuta na gesi baharini, shughuli za ufugaji wa bahari ikiwa ni pamoja na samaki na ufugaji wa mwani baharini na pwani, utalii, meli na usafiri wa baharini ikijumuisha miundombinu na huduma zinazohusiana.

Ndani ya ukanda wa pekee wa kiuchumi, mataifa yanadai haki ya kutumia eneo la bahari kwa madhumuni ya kushiriki katika uvuvi endelevu, uchunguzi na utafiti wa rasilimali za baharini na matumizi endelevu ya bahari, kuhifadhi na kusimamia maliasili hai na zisizo hai za maji yaliyo karibu na chini ya bahari. Shughuli zingine zinazofanyika katika eneo pekee la kiuchumi ni kuzilinda rasilimali zinazoweza kurejeshwa nje ya nchi kutokana na mawimbi, mikondo, na upepo. Kama nchi iliyopo ukanda wa Pwani, Tanzania ina mamlaka kamili juu ya eneo lake la bahari na maji ya ndani.

Ili kuwa na usalama na ulinzi wa mazingira ya baharini katika eneo la bahari na maji ya maji ya ndani na kuimarisha ulinzi wa rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu ya kitaifa, Serikali inahitaji uwezo wa kukabiliana moja kwa moja na vitendo vya kihalifu baharini. Mara zote katika kushugulikia maswala haya yanajumumisha vyombo vingi ili kupata ufanisi katika utekelezaji wa ulinzi na usalama wa baharini na unachangiwa zaidi na mifumo ya jumla ya uratibu wa kitaifa yenye mwingiliano wa majukumu. Shughuli haramu za baharini mara nyingi hujumuisha mamlaka ya vyombo vingi. Hivyo, kuunda njia za kutegemewa za mawasiliano na uratibu wa hatua kati ya taasisi ni muhimu kwa ajili ya kukabiliana na shughuli haramu za majini hususani kwenye maziwa na bahari.

Suluhisho za muda mrefu za changamoto zinazohusiana na shughuli haramu za baharini hazipo katika nyanja moja. Katika mazingira ya baharini yanayozidi kuwa na mitandao yenye sura nyingi jitihada za pamoja za Serikali zinahitajika ili kukabiliana na suala hili. Kuanzisha Kikosi cha kuhamasisha kupiga vita dhidi ya shughuli haramu za baharini ni mbinu muhimu ya kukabiliana na matukio haramu baharini.

Madhumuni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuanzisha na kuimarisha utaratibu mpana na wa kina wa kusimamia shughuli za usalama wa baharini ili kuimarisha kwa haraka na kuzuia matukio ya uvuvi haramu, yasiyoripotiwa na yasiyodhibitiwa, ajali za baharini zisizotabirika, matukio ya uchafuzi wa baharini, magendo, na usafirishaji haramu.

1.2 Matarajio ya mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia matarajio kuhusu kukabiliana na shughuli haramu za baharini katika mazingira ya eneo la bahari la kitaifa na maji ya ndani kwa miaka mitatu ijayo kama ifuatavyo:-

(a) Tanzania itaendelea kupambana na wahalifu wa ndani, kikanda na watu binafsi na vikundi vya wahalifu ambao wako tayari kuhatarisha matumizi ya eneo la bahari kama njia ya kusafirisha nyenzo haramu zinazohusiana na shughuli haramu za kawaida zilizotajwa.

(b) Kuwepo kwa maliasili nyingi nchini Tanzania zikiwemo samaki, wanyamapori na mazao ya misitu zitaendelea kuvutia shughuli haramu katika eneo la bahari.

(c) Eneo la kijiografia la Tanzania linaifanya nchi kukabiliwa na vitisho vya ugaidi kutoka baharini na uharamia na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na magendo ya wahamiaji kama njia ya kupitia.

(d) Utamaduni wa upashanaji habari utaendelezwa ndani ya nchi, kimataifa, na mashirika yote ya kimataifa yanayoshiriki katika eneo hili ambayo yanahitaji kufanya kazi pamoja ili kukabiliana na shughuli haramu za baharini.

(e) Kanuni na Taratibu za Uendeshaji na utekelezaji wa mwongozo zitatayarishwa na kutumika.

(f) Sheria ya Kitaifa ya Utafutaji na Uokoaji itatungwa ili kuwezesha utayarishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utafutaji na Uokoaji ambao utasaidia katika kuongeza utayari na mwitikio wa mahitaji ya utafutaji na uokoaji nchini.

(g) Rasilimali za kutosha zitawekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mwongozo na kila chombo/taasisi inayohusika.

(h) Tathmini ya mahitaji ya mafunzo itafanywa na programu ya mafunzo itatayarishwa na kutekelezwa kwa ajili ya utekelezaji bora wa mwongozo huu.

(i) Sera na sheria husika zitapitiwa upya na kuhuishwa ili kuwezesha utekelezaji wa mwongozo huu.

(j) Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Baharini utaandaliwa.

2. MAONO, UPEO NA LENGO LA MWONGOZO

2.1 Maono

Kukuza uratibu baina ya taasisi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuelekea maji salama, ulinzi na mazingira bora ya bahari na maji ya ndani.

2.2 Upeo

Mwongozo huu unazingatia usalama wa majini ya ndani, ulinzi wa mazingira na matumizi haramu katika maji hayo.

2.3 Malengo na maeneo ya kipaumbele

2.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu ni kuweka mfumo madhubuti wa uratibu wa vyombo vya Serikali vinavyohusika na udhibiti, ulinzi na usalama wakati wa kushughulikia shughuli haramu za baharini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Malengo mahususi ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuimarisha matumizi bora ya rasilimali na taasisi zinazowajibika za Serikali zinazoshiriki kukabiliana na shughuli haramu za baharini kwa kuunganisha rasilimali kwa lengo la kutumia rasilimali hizo ili kupata matokeo bora zaidi.

(b) Kuweka utaratibu wa uratibu wa kitaasisi wa kushughulikia shughuli haramu za baharini nchini.

(c) Kuimarisha upashanaji wa habari au mfumo wa utoaji taarifa kuhusu shughuli haramu za baharini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(d) Kusaidia hatua za utekelezaji wa mikataba inayotumika ya kikanda na kimataifa iliyosainiwa au kuridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.3.2 Maeneo ya kipaumbele

Maeneo ya kipaumbele ya mwongozo huu ni kama ifuatavyo: -

(a) Kukomesha na kuzuia Tanzania kuwa njia ya kuingiza na kutoa mihadarati.

(b) Kuzuia biashara ya nyara za Serikali.

(c) Kuzuia Tanzania isitumike kama njia ya kusafirishia wahamiaji haramu na kupiga vita biashara haramu ya binadamu.

(d) Kuzuia na kukomesha uingiaji wa bidhaa zisizo na kiwango au usafirishaji wa bidhaa hizo.

(e) Kukabiliana na ajali za majini ndani ya ukanda wa Tanzania.

(f) Kulinda Bandari za Tanzania dhidi ya matishio ya usalama.

(g) Kuzuia na kukabiliana na uvuvi haramu katika ukanda maalum wa kiuchumi wa Tanzania.

(h) Kulinda shughuli za utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

3. SHUGHULI HARAMU KATIKA UKANDA WA BAHARI NA MAJI YA NDANI

3.1 Shughuli haramu zinazofanyika

Tanzania inakabiliwa na kundi kubwa la shughuli haramu zinazotokana na watendaji mbalimbali katika eneo la bahari na maji ya ndani. Shughuli haramu za kawaida za baharini zinazoikabili Tanzania ni pamoja na biashara ya dawa za kulevya, uvuvi haramu usioripotiwa usiodhibitiwa, biashara haramu ya binadamu/usafirishaji wa wahamiaji haramu, utoroshaji wa maliasili (wanyamapori, misitu na gesi asilia), uchafuzi wa bahari na uharibifu wa mazingira, uhalifu wa mtandaoni, uhalifu unaohusiana na vitambulisho, dawa za kulevya, ajali za baharini na vitisho vya usalama dhidi ya bandari. Kwa

kuzingatia eneo la kijiografia la eneo la bahari ya Tanzania na maji ya ndani, shughuli nyingi haramu za baharini zilizotajwa hapo juu zinaweza kuainishwa kama uhalifu wa kupangwa wa kimataifa.

3.2 Kupunguza shughuli haramu bahari na maji ya ndani

Ili kulinda, kukabili na kupunguza shughuli haramu, vyombo/taasisi husika zitazingatia yafuatayo:-

(a) Kuimarisha ufuatiliaji, udhibiti na doria katika eneo la bahari.

(b) Kukuza ufahamu wa usalama wa bahari na kubadilishana habari.

(c) Kuimarisha hatua za udhibiti (uchunguzi wa vyombo na vyeti, utoaji wa leseni, utoaji wa vibali, nk).

(d) Kujenga uwezo kupitia ajira na mafunzo ya wafanyakazi katika wakala au taasisi husika.

(e) Kufanya mazoezi ya pamoja ya nadharia na vitendo.

(f) Kuimarisha taratibu za kukamata na kuwafungulia mashtaka wahalifu katika mahakama za sheria zenye mamlaka ya kushughulikia na kuamua masuala ya baharini.

4. URATIBU

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatumia uwezo wake kuchukua hatua jumuishi katika wigo wa kupambana na shughuli haramu za baharini. Uratibu chini ya mwongozo huu unazingatia sera, sheria, weledi, upashanaji habari na uwajibikaji wa pamoja. Uratibu wa kazi za kukabiliana na shughuli haramu katika bahari na maji ya ndani utafanyika kama ifuatavyo:-

4.1 Sera na Sheria

Sera na sheria za kitaifa pamoja na mikataba ya kikanda na Kimataifa itatoa mwongozo wa utekelezaji wa mfumo huu. Orodha yenye baadhi ya vipengele vya Sera za Kitaifa, Sheria na Mikataba ya Kimataifa ipo kwenye Kiambatisho Na. 1.

4.2 Kubadilishana habari na uzoefu

Kubadilishana habari ni msingi bora wa uratibu. Kuanzisha na kuendelea na utaratibu rasmi wa kubadilishana habari ni muhimu kwa mashirika na taasisi za umma na kimataifa.

Kituo cha Kupokea na Kutoa habari kwa madhumuni ya mwongozo huu kitaanzishwa. Kituo kitakuwa na taratibu zake za kuwasilisha taarifa kwa taasisi na wakala husika wa utendaji kazi kwa ajili ya kuzitolea majibu. Kituo hiki kitakuwa katika Kituo cha Uratibu wa Uokoaji Majini kilichopo Dar es Salaam (MRCC) na kitafanya kazi kwa karibu na Kituo cha Ufuatiliaji wa Uvuvi (FMC) ambacho kinawajibika kwa kufuata mahitaji yote ya kutoa taarifa za meli za uvuvi, mfumo wa ufuatiliaji wa meli na uthibitishaji wa hati za takwimu kwa mashirika ya kikanda ya usimamizi wa uvuvi.

4.3 Shughuli za pamoja

Shughuli za pamoja kama hitajio linapotokea zitakuwa ni kipengele muhimu cha utekelezaji wa mwongozo huu. Operesheni hizi zitaendeshwa na Taasisi tofauti kulingana na Taarifa zilizopokelewa na majibu yanayohitajika.

Uratibu wa shughuli za usalama na kuzuia uchafuzi utakuwa chini ya Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) na shughuli za uratibu zitajumuisha utafutaji na uokoaji, usalama wa meli na bandari, ulinzi wa mazingira ya baharini, kugundua na kukabiliana na umwagikaji wa mafuta (chini ya Mpango wa Kitaifa wa Dharura wa Kumwagika kwa Mafuta ya Baharini), uokoaji na matibabu kwenye meli na ununuzi wa vifaa na mitambo ya mawasiliano baharini.

Fedha za mafuta kwa ajili ya shughuli za pamoja za baharini na majini kwa ajili ya kukabiliana na shughuli haramu za baharini zitatengwa kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mafuta kwa ajili ya shughuli hizo yatahifadhiwa chini ya mipango maalum na Wakala wa Manunuzi ya Umma Serikalini (GPSA) na yatapatikana kwa matumizi wakati wote. Ofisi ya Waziri Mkuu itaandaa taratibu za upatikanaji wa mafuta hayo kwa wakati kwa vyombo husika vinavyofanya operesheni zinazohusiana na kukabiliana na shughuli haramu za baharini.

4.4 Mazoezi ya pamoja

Mazoezi ya Taasisi na Wakala mbalimbali yataendeshwa na mashirika yanayoshiriki ili kupima kiwango cha kujiandaa na kukabiliana na shughuli haramu za kitaifa na kimataifa. Mazoezi haya yanaweza kuwa ya mezani au ya vitendo ambayo yatafanywa kila mwaka na miaka miwili mtawalia.

Ofisi ya Waziri Mkuu itaratibu mazoezi hayo kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazohusiana na shughuli za bahari na maziwa makuu na zitatengenezwa taratibu na kanuni za uendeshaji (SOP) zinazoelezea jinsi mazoezi yatakavyofanyika.

Rasilimali fedha zinazohitajika kutekeleza mazoezi ya taasisi na wakala mbalimbali zitatolewa na mamlaka za kitaifa au mashirika yanayohusika na usafiri wa baharini, bandari, huduma za misitu, mafuta na gesi, uvuvi wa bahari kuu, na udhibiti na uhalifu wa madawa ya kulevya.

4.5 Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Baharini

Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Baharini utakapoandaliwa utatoa mwongozo zaidi juu ya utekelezaji wa mfumo huu. Mkakati huo utaakisi masilahi ya kitaifa ya usalama wa baharini na udhaifu wake na kuweka malengo ya pamoja na kufafanua hatua zinazolenga kuelekeza matumizi ya njia zote zilizopo ili kutimiza malengo hayo.

5. USIMAMIZI WA MWONGOZO

5.1 Msimamizi mkuu

Ofisi ya Waziri Mkuu itakuwa msimamizi wa mwongozo na itatoa maelekezo ya jumla kuhusu utekelezaji kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Taifa ya Usimamizi na

kushirikisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa maeneo yanayohitaji utendaji wa pamoja.

Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo itajumuisha Katibu Mkuu - Ofisi ya Makamu wa Rais, Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais TAMISEMI, Katibu Mkuu - Ofisi ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu wa Wizara zenye dhamana na Ulinzi, Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani, Fedha, Usafiri wa Baharini/Uchukuzi, Sheria na Masuala ya Katiba, Serikali za Mitaa, Uvuvi, Utalii, na Maliasili kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT). Kamati itaongozwa na Katibu Mkuu - Ofisi ya Waziri Mkuu na itapokea taarifa za tathmini kutoka kwenye Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini (NMSC) kupitia kwa Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Usafiri wa Majini mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya kuzingatiwa mwongozo wa utekelezaji wa muundo huu ili uweze kufikia malengo yake.

Fedha kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na utekelezaji wa mwongozo huu zitatengwa katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiutawala zinazohitajika ikijumuisha kuwezesha mikutano ya Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwomgozo na utoaji wa maelekezo na maagizo ya jumla juu ya utekelezaji wa mwongozo.

5.2 Majukumu na Wajibu wa Kamati yaTaifa ya Usalama wa Baharini

Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini itakuwa na majukumu yafuatayo chini ya mwongozo huu; -

(a) Kuweka mahitaji kwa ajili ya kujitathmini kwa vyombo vinavyoshiriki ili kupima mafanikio ya malengo ya mwongozo huu.

(b) Kupokea na kukagua taarifa za kujitathmini kutoka kwa vyombo vinavyoshiriki.

(c) Kutathmini ya utekelezaji wa mwongozo huu itatolewa kila baada ya miezi sita ili kubaini mafanikio ya malengo yake kwa kuzingatia taarifa za utekelezaji kutoka katika taasisi zinazoshiriki katika utekelezaji wa mwongozo huu.

(d) Kuwasilisha taarifa kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Usafiri wa Majini tathmini zenye mapendekezo kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo huu.

(e) Kufanya mapitio ya mwongozo huu kila baada ya miaka mitatu na kuwasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Usafiri wa Majini. Taarifa hiyo itatoa mapendekezo kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo.

(f) Kuandaa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji zinazoelezea jinsi operesheni za pamoja zitakavyofanyika.

5.3 Wajibu na majukumu ya vyombo vingine

Katika kutekeleza mwongozo huu, wajibu na majukumu yatakayotekelezwa na taasisi na wakala husika kwa kuzingatia majukumu yao ni kama ifuatavyo:

5.3.1 Shirika la Wakala wa Meli Tanzania na Kituo cha Kupashana Habari

(a) Kuandaa mipango ya awali ya kujiandaa na kukabiliana na shughuli haramu za baharini na kuhakikisha kuwa taarifa za kijasusi zinapokelewa kama zilizofafanuliwa katika kifungu cha 3 zinazingatiwa na Kituo cha Kupashana Habari.

(b) Kuandaa na Kusimamia matukio ya kila robo mwaka ya shughuli zilizoratibiwa na Wakala. Matukio haya ya uratibu yanapaswa kuhusisha miongoni mwa mambo mengine mapitio ya shughuli zilizofanyika katika robo iliyopita, shughuli zilizopangwa za robo ijayo, matukio yanayotarajiwa ya ngazi ya kitaifa katika robo ijayo, na kupokea taarifa kutoka kwa mashirika au taasisi zinazoshiriki katika utekelezaji wa mwongozo huu.

(c) Kuandaa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji ambazo zinasimamia taratibu za utoaji wa taarifa.

(d) Kukusanya taarifa za kijasusi za baharini na takwimu kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mashirika yanayohusika na utekelezaji wa mwongozo huu.

(e) Kuchambua na kusambaza taarifa na takwimu zilizopokelewa kutoka kwenye vyanzo mbalimbal vya kuaminika kwa Wakala husika wa utendaji kwa ajili ya kukabili na kuchukua hatua na kumfahamisha msimamizi wa mwongozo huu kama inavyofaa.

(f) Kutunza daftari (Taarifa) za shughuli haramu za baharini zinazofanyika nchini.

(g) Kuwezesha tathmini ya utendaji kazi za mwongozo kupitia Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini na kuwasilisha taarifa za tathmini kwa Wizara yenye dhamana ya usafiri wa baharini.

(h) Kusaidia mipango ya uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji endelevu wa mwongozo.

(i) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za mwongozo kwa kuzingatia mahitaji ya tathmini ya Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini ili kubaini mafanikio ya malengo ya mwongozo na kuwasilisha ripoti ya tathmini kwenye Kamati hiyo.

5.3.2 Mashirika ya Utekelezaji wa Sheria ya Bahari

Mashirika yanayohusika na utekelezaji wa Sheria ya Bahari yameorodheshwa katika Kiambatisho Na. 2. Mashirika hayo yatakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kutoa taarifa muhimu kwa wakati kwa Kituo cha Kupashana Habari kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji.

(b) Kutoa Maafisa wa Uhusiano kwa Kituo kama inavyohitajika.

(c) Kuchukua hatua za kukabili kutokana na taarifa zilizopokelewa kutoka kwenye Kituo cha Kupashana Habari.

(d) Kutunza mali na vifaa vya kukabiliana na hali hiyo na kuweka rasilimali watu ya kutosha katika hali inayoendelea ya utayari wa kukabiliana na shughuli haramu za baharini.

(e) Kufanya tathmini ya shughuli za mwongozo kwa kuzingatia mahitaji ya tathmini ya Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini ili kubaini mafanikio ya malengo ya mwongozo na kuwasilisha taarifa ya tathmini kwenye Kamati hiyo.

(f) Kulinda eneo la uhalifu au tukio na kuhakikisha ulinzi na usalama wa timu unakuewepo wakati wote wa shughuli.

(g) Kufanya upekuzi na ukamataji kwa mujibu wa sheria zinazotumika.

(h) Kukamata na kuhoji watuhumiwa na kurekodi taarifa za watuhumiwa na mashahidi.

(i) Kukusanya majalada ya kesi na kuyawasilisha kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya maamuzi.

5.3.3 Mashirika mengine yanayoshiriki

Mashirika mengine yanayotekeleza shughuli zake katika katika ukanda wa bahari na maziwa makuu (Kiambatisho Na. 3) yatakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kutoa taarifa muhimu zinazohusika kwa wakati kwenye Kituo cha Kubadilishana Taarifa kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji.

(b) Kutoa Maafisa wa Uhusiano kwenye Kituo cha Kupashana Habari kama inavyohitajika.

(c) Kuunga mkono na kushiriki katika hatua za kukabiliana na uhalifu na vyombo vya kutekeleza sheria kutokana na taarifa au ombi lililowasilishwa kwenye Kituo kama inavyofaa.

(d) Kufanya tathmini ya shughuli za mwongozo kwa kuzingatia mahitaji ya tathmini ya Kamati ya Taifa ya Usalama Baharini ili kubaini mafanikio ya malengo ya mwongozo na kuwasilisha taarifa kwenye Kamati hiyo.

(e) Kusaidia mipango ya uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji bora na endelevu wa mwongozo huu

MUUNDO WA USIMAMIZI WA MWONGOZO



6.3 Maandalizi ya Kanuni na Taratibu za Uendeshaji

Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini itahakikisha uwepo wa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na uhakiki wa mwongozo huu.

6. UFUATILIAJI, TATHMINI NA MAPITIO YA MWONGOZO

6.1 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini utatumika kutathmini utekelezaji wa mwongozo kwa lengo la kuboresha usimamizi wa matokeo na athari. Madhumuni ya ufuatiliaji yatakuwa ni kubaini iwapo uratibu na mpango kazi unaotarajiwa umefikiwa ili hatua zichukuliwe kurekebisha kasoro hizo haraka iwezekanavyo.

Tathmini ya mwongozo huu itafanywa ili kupima kama matokeo yaliyotarajiwa yalipatikana ikiwa matokeo mengine yasiyotarajiwa yatazingatiwa na kama mwongozo huu ulitoa mchango wa maana, thabiti wa kudumu na kwa gharama nafuu kwa kutumia mbinu ya uratibu wa pamoja na michakato ya maendeleo ya kitaifa.

Ufuatiliaji wa mwongozo huu utaendelea kufanyika kwa kutumia Kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Baharini wakati tathmini ya mfumo huu itafanywa na Kamati hiyo baada ya kupokea taarifa za kujitathmini za wakala binafsi. Tathmini hiyo itafanyika kila baada ya miezi sita na taarifa yake kuwasilishwa kwenye Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo huu. Taarifa hiyo itazingatia mambo yafuatayo:

(a) Kuweka malengo yanayokusudiwa kufikiwa na mwongozo huu.

(b) Kutathmini ni kwa kiasi gani malengo hayo yanafikiwa.

(c) Kutathmini ikiwa malengo hayo yanafaa kuendelea kutumika na kiwango ambacho yanaweza kufikiwa zaidi kupitia uratibu wa pamoja ulioimarishwa zaidi.

6.2 Mapitio ya Mwongozo

Mwongozo huu utapitiwa upya na Kamati ya Taifa ya Usalama wa Baharini kila baada ya miaka mitatu au kama hitajio linapotokea kabla ya mwisho wa miaka mitatu kufuatia matukio muhimu. Madhumuni ya uhakiki huo ni kuhakikisha kuwa malengo ya mwongozo huu yanafikiwa na kufanyiwa mapitio kwa wakati kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya taifa, kikanda na kimataifa.

Taarifa ya mapitio yenye mapendekezo itawasilishwa na Kamati ya Taifa ya Usalama Baharini kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya usafiri wa majini ili yawasilishwe kwenye Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo huu kwa ajili ya kuzingatiwa. Mapendekezo hayo yatajumuishwa katika taarifa ya mapitio ya mwongozo yataamuliwa na Kamati ya Taifa ya Usalama Baharini na kuidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Mwongozo.

Kiambatisho cha 1: Orodha ya vyenzo zinazohusika kwa utekelezaji wa mwongozo

(a) Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999.

(b) Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007.

(c) Sera ya Taifa ya Misitu ya 1998.

(d) Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015.

(e) Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997.

(f) Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004.

(g) Sera ya Taifa ya Usafiri ya 2003.

(h) Sera ya Usalama wa Taifa ya 2008.

(i) Sheria ya Petroli namba 21 ya mwaka 2015.

(j) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 5 ya 2009.

(k) Sheria ya Misitu Na.14 ya 2002.

(l) Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 RE 2016.

(m) Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 na Kanuni zake za 2010.

(n) Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania namba 14 ya mwaka 2017 na Kanuni ya Udhibiti wa Jimbo la Bandari ya mwaka 2019.

(o) Sheria ya Usafirishaji Meli kwa Wafanyabiashara namba 21 ya mwaka 2003 na Kanuni zake.

(p) Sheria ya Usafiri wa Majini Na. 5 ya mwaka 2006.

(q) Sheria ya Mamlaka ya Bandari Tanzania namba 17 ya mwaka 2004.

(r) Sheria ya Ulinzi wa Taifa namba 24 ya mwaka 1966.

(s) Sheria ya Nishati ya Atomiki Na. 7 ya 2003.

(t) Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Mashtaka, Sura ya 430 RE 2019.

(u) Sheria ya Uchumi wa Eneo la Pekee (EEZ) namba 3 ya mwaka 1989.

(v) Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 RE ya 2020 na Kanuni zake za 2021

(w) Sheria ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009.

(x) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 20 ya mwaka 2004.

(y) Sheria ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Namba 2 ya mwaka 2010.

(z) Sheria ya Dawa za Kulevya na Kuzuia Dawa za Kulevya, Namba 9 ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2011 na 2019.

(aa) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, namba 5 ya mwaka 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2017.

(bb) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu namba 6 ya mwaka 2008.

(cc) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 RE 2019.

(dd) Sheria ya Usalama wa Taifa Sura ya 47 RE 2002.

(ee) Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, 2019.

(ff) Mkataba wa Kikanda wa Bandari (PSMA), 2009.

(gg) Mkataba wa Ardhi oevu zenye Umuhimu wa Kimataifa hasa kama Makazi ya Ndege wa Majini (Mkataba wa RAMSAR, 1971).

(hh) Mkataba wa biashara ya kimataifa ya spishi zilizo hatarini kutoweka za Mimea na Fauna (1973).

(ii) Mpango wa Kimataifa wa Utekelezaji wa kukabiliana na uvuvi wa IUU (IPOA –IUU, 2001).

(jj) Mkataba wa Cape Town kuhusu usalama wa Meli za Uvuvi, (CTA 2012).

(kk) Mkataba wa Kimataifa wa Viwango vya Mafunzo, Uidhinishaji na Utunzaji wa Mifugo ya Uvuvi (STCW-F ya 1995).

(ll) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari (UNCLOS ya 1982).

(mm) Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu uliopangwa wa Kimataifa, 2000.

Kiambatisho cha 2: Orodha ya Wizara, Idara, na Taasisi Zinazohusika katika Utekelezaji wa Sheria za Baharini

(a) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania - Kamandi ya Jeshi la Wanamaji.

(b) Jeshi la Polisi Tanzania – Polisi Wanamaji.

(c) Idara ya Usalama Tanzania (TISS).

(d) Huduma za Kitaifa za Mashtaka (NPS).

(e) Wizara ya Mambo ya Ndani – Idara ya Uhamiaji.

(f) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Forodha.

(g) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Kiambatisho cha 3: Orodha ya Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika Mengine yanayoshiriki katika utekelezaji

(a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Idara ya Uvuvi.

(b) Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC).

(c) Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari ya Kina (DSFA).

(d) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

(e) Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

(f) Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

(g) Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya.

Kiambatisho cha 4: Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mwongozo

S/N	Shughuli	Mhusika	Muda
01	Kupitia sera na sheria zinazohusu utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uratibu wa Kukabiliana na Shughuli Haramu za Baharini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Rejea 4.1)	Wizara mbalimbali zinazohusika kwa mujibu wa sera na sheria zinazotumika, Wizara ya Sheria na Katiba	Muda wa kati
02	Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Baharini. (Rejea 4.5)	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi	Muda mfupi
03	Kituo cha Kubadilishana Taarifa kitafanya kazi chini ya Kituo cha Operesheni na Uokozi wa Majini (MRCC) Dar es Salaam. (Rejea 4.2)	Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC)	Muda mfupi
04	Ofisi ya Waziri Mkuu kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa shughuli za wakala zinazohusiana na kukabiliana na shughuli haramu za baharini na taasisi husika kuchangia bajeti ya mafuta. (Rejea 4.3)	Ofisi ya Makamu wa Rais, TPA, TASAC, DSFA, TRA, TFS, DCEA	Muda mfupi
05	Kununua Vifaa vya Uendeshaji: (a) Kamera, Mfumo wa dharura wa mawasiano na Usalama wa Bahari Ulimwenguni (GMDSS), Kituo cha Redio, Zana za Picha za Uendeshaji za Kawaida (COP). (b) Gari lisiokuwa na rubani (UAV - Drone), Magari na Ndege, Mfumo wa Kitambulisho Kiotomatiki (AIS), mfumo wa Data & utunzaji. (c) Boti za Doria, Vipuri vya Helikopta, Mikataba ya huduma za Matengenezo.	Vyombo vya usalama vinavyohusika na utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uratibu wa Kukabiliana na Shughuli Haramu za Baharini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TASAC (MRCC).	Muda wa kati na mrefu
06	Kuanzisha Kituo cha Uratibu na Uendeshaji wa Shughuli za Majini Ndani ya Nchi.	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.	Muda mrefu
07	Kutenga fedha kwa ajili ya gharama za utekelezaji katika bajeti ya Serikali. (Kumb.5.1)	Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha na Mipango	Muda mfupi

08	Kuratibu na kufanya mazoezi ya pamoja ya nadharia na vitendo. (Rejea 4.4)	Ofisi ya Waziri Mkuu na mashirika mengine yanayohusika	Muda mfupi
09	Kufanya Shughuli za Pamoja. *(Rejea 4.3)*	Wakala zote za Utekelezaji	Muda mfupi
10	Kuandaa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa kufanya shughuli za pamoja. (Rejea 4.3)	Kamati ya Taifa ya Usalama Baharini (NMSC)	Muda mfupi
11	Kuandaa Kanuni na taratibu za Uendeshaji na kufanya mazoezi na wadau wa bahari mbalimbali. (Rejea 4.4)	Ofisi ya Waziri Mkuu na mashirika mengine yanayohusika	Muda mfupi
12	Kuandaa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji ambazo zinasimamia utoaji wa taarifa kwenye Kituo cha Kubadilishana Taarifa (ISC). (Rejea aya.5.3.1 (iii))	Ofisi ya Waziri Mkuu na mashirika mengine yanayohusika	Muda mfupi
13	Kuandaa Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa Ufuatiliaji, Tathmini na Mapitio ya Mfumo wa Mwongozo wa Taifa wa Uratibu wa Kukabiliana na Shughuli Haramu za Baharini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Rejea aya.6.3)	NMSC	Muda mfupi
14	Kuweka mahitaji ya kujitathmini kwa vyombo vinavyoshiriki ili kupima mafanikio ya malengo ya mwongozo. (Rejea aya.5.2)	NMSC	Muda mfupi
15	Kuandaa mipango ya awali ya kujiandaa na kukabiliana na shughuli haramu za baharini na kuhakikisha kuwa taarifa za kijasusi zinapokelewa na Kituo cha Kubadilishana habari. (Rejea aya.5.3.1)	Ofisi ya Waziri Mkuu na mashirika mengine yanayohusika	Muda mfupi
16	Kuandaa taratibu za kupata taarifa za jumla kwenye taarifa ya ukaguzi. (Rejea aya.6.2)	NMSC	Muda mfupi
17	Kuandaa taratibu za upatikanaji wa mafuta kwa wakati kwa vyombo husika vinavyofanya kazi. (Rejea aya.4.3)	Ofisi ya Waziri Mkuu na mashirika mengine yanayohusika	Muda mfupi

UHURU
NA
UMOJA